# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

*Dar es Salaam*
*20 Septemba, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

## TAARIFA KWA UMMA
### RAIS SAMIA AKUTANA NA MAKAMU WA RAIS MSTAAFU WA UGANDA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo, tarehe 20 Septemba, 2026, amekutana na kufanya mazungumzo na Makamu wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Uganda, Mheshimiwa Dkt. Speciosa Wandira Kazibwe.

Katika mazungumzo yao yaliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam, viongozi hao wamezungumzia umuhimu wa mshikamano miongoni mwa viongozi wanawake na nafasi yao katika kuleta mabadiliko ya kijamii.

Aidha, wamejadili mchango wa viongozi wanawake katika kuhamasisha ushiriki wa wanawake kwenye nafasi za uongozi na maamuzi, pamoja na kuchochea maendeleo endelevu katika jamii.

Dkt. Kazibwe alikuwa Makamu wa Rais wa Uganda kuanzia mwaka 1994 hadi 2003, na mwanamke wa kwanza barani Afrika kushika wadhifa huo.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu